# ACHIEVERS FOCUS EXAMINATION SERIES

WEGO PUBLISHERS
The achievers focus

## STANDARD 8 – 2021

## KISWAHILI

AF005

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Zipo aina tatu za familia. Ipo ile ya asilia __1__ baba, mama na watoto. __2__ ni ile ya __3__ ambayo kwayo humpata mume mmoja akioa wake zaidi ya mmoja na watoto kadhaa. __4__ ipo nyingine iitwayo familia panuzi. Hii panuzi huhusisha watoto, wazazi, babu, bibi, hau, amati, hale, wapwa na wengine wengi. Jambo ambalo ni __5__ katika familia zote ni kupendana, kuelewana __6__ katika gange yoyote __7__. Itokeapo shida ni sharti kama __8__ wahusika waketi pamoja wasemezane ili kupata suluhu. Kumbuka kuwa matatizo katika familia yapo lakini ni muhimu kuzingatia kuwa bila ya kuelewana na kushirikiana kama __9__, basi kwa hakika familia itasambaratika. Aisee!

**1.** A. ambayo inayojumuisha
B. ambayo ijumuishayo
C. ambayo inajumuisha
D. ambao inaojumuisha

**2.** A. Zingine B. Ingine
C. Nyingine D. Nyinginezo

**3.** A. mitara B. ukazawana
C. jamii D. jumla

**4.** A. Mathalani B. Madhalani
C. Licha ya D. Mbali na hizo

**5.** A. muhali B. izara
C. aula D. auni

**6.** A. kupigana kumbo B. kupeana mkono
C. kulambana kisogo D.kulilia ngoa

**7.** A. zifanywazo B. iletwayo
C. zifanywayo D. ifanywayo

**8.** A. ibada B. kaburi
C. barafu D. ardhi

**9.** A. kiko na digali B. mafuta na maji
C.ardhi na mbingu D. maziwa na tui

**10.** A. akili ni nywele
B. tenda wema nenda zako
C. mfinyanzi hulia gaeni
D. kinga na kinga ndipo moto uwakapo

Kukutana kwangu naye kulikua kwa sadfa. Nilikuwa __11__ mgundani __12__. __13__, mara nikamwona kijana Amani __14__ barasteni. Hali yake ilisikitisha kutokana na __15__ ulevi haramu.

**11.** A.ninaelekea B. naelekea
C. nikielekea D. nilielekea

**12.** A. kunadi B. kuabudu
C. kuinjika D. kupogoa

**13.** A. Mvua ulikua ukinyesha B. Kulikua kukinyesha
C. Mvua ilikua ikinyesha D. Mvua zilikuwa zikinyesha

**14.** A. akipepesuka B. akihohusa
C. akiwewesuka D. akitweta

**15.** A. kunywa B. kulewa
C. kushiriki D. kutopea

**Kutoka swali 16 – 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.**

**16.** Ni kundi lipi lenye vimelea pekee?
A. Utitiri, chawa, funza, kiroboto
B. Kinegwe, kirinimbi, kinyemere, kigwena
C. Siafu, komba, nondo, kipepeo
D. Mbayuwayu, tekenya, kupe, tai

**17.** Neno lipi limeambatanishwa sawasawa na ngeli yalo?
A. Kitoto A – WA B. Chura KI – VI
C. Mahusiano U – YA D. Manyoya YA – YA

**18.** Onyesha usemi halisi wa sentensi ifuatayo.
Muli aliniambia ya kwamba wiki ambayo ingefuata angeenda kutazama mechi hiyo.
A. "Wiki ambayo ilipita ulienda kutazama mechi hiyo." Muli akaniambia
B. "Wiki ijayo nitaenda kutazama mechi hiyo." Muli akaniambia
C. "Wiki ijayo nitaenda kutazama mechi hiyo." Muli akaniambia
D. "Wiki ambayo ilifuata nilienda kutazama mechi hiyo." Muli akaniambia

**19.** Maana ya "**tia mrija**" ni
A. kutumia mali vibaya
B. kujitafutia mali kwa hila
C. kumtegemea mtu kwa kila kitu
D. kumchukulia mtu mali ya mwenzake

**20.** Ni neno lipi lenye sauti mwambatano?
A. Wayo B. Kunjika
C. Msumeno D. Nyanya

**21.** Kanusha sentensi ifuatayo :
'Gari lililoanza safari limeanguka'
A. Gari lililoanza safari halikuanguka
B. Gari halikuanza safari wala kuanguka
C. Gari lisiloanza safari limeanguka
D. Gari lililoanza safari halikuanguka

**22.** Sentensi '**Ukumbi ulimeza sisisi ya watu**' imetumia tamathali gani ya usemi?
A. Chuku B. Tashihisi
C. Tashbiha D. Jazanda

**23.** Yupi hawezi kuwa nyanya yangu?
A. Bibi ya binamu yangu
B. Mama ya shangazi wangu
C. Bibi ya babu yangu
D. Nyanya ya mpwa wangu

**24.** '**Ka**' imetumikaje katika sentensi:
Mvulana aliwasili nyumbani, akavua nguo, akafululiza jikono, akala?
A. Kuonyesha hali ya kuendeleza kwa matukio
B. Kuonyesha hali ya wakati uliopita
C. Kuonyesha hali ya kufuatana kwa matukio
D. Kuonyesha hali ya kusudi

**25.** "Gao huwa chombo wakatiwe" ni kwa wanaovidharau vitu vikuu; "Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno" ni kwa wale
A. Wanaovidharau vitu vidogo
B. Wanaopuuza msaada mkubwa
C. Wanaupuuza mali ya wengine
D. Wanaotumia mali ya wengine

**26.** Maneno yaliyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo ni?
Mzazi <u>wangu</u> amefika lakini <u>wako</u> atafika kesho.
A. Kuvumishi, kielezi B. Kiwakilishi, kivumishi
C. Kielezi, kiwakilishi D. Kivumishi, kiwakilishi

**27.** Kamilisha kwa ufasaha:
Mtoto huyu, huyo na yule _____
A. mnifuate B. wanifuate
C. tufuate D. anifuate

**28.** Andika tarakimu 10001 kwa maneno ni?
A. Elfu kumi na moja B. Elfu kumi na mia moja
C. Kumi elfu na moja D. Kumi elfu na sufuri moja

**29.** Musa alipokuwa akitoka shuleni wakati wa jioni, kivuli chake kilikuwa nyuma yake. Je, shule ilikuwa upande gani wa dira?
A. Magharibi B. Mashariki
C. Kusini D. Kaskazini

**30.** Akisami hii huitwa vipi? $\frac{5}{6}$
A. Khumusi sita B. Sudusi khumusi
C. Sudusi tano D. Subui tano

**Soma kifungu kufuatacho kisha jibu maswali 31 – 40.**

Bila shaka umewahi kusikia neno mwalimu likitajwa. Je, neno hilo linapotajwa ni wazo gani hukujia akilini? Yumkini huenda ukaniambia mwalimu ni yule anayekufunza masomo mbalimbali darasani. Wengine huenda wakasema mwalimu ni mtu ambaye anawarithisha wengine maarifa; yawe ya darasani ama nje ya darasa. Almuradi kila binadamu anaweza kutoa maana anawai ya neno kulingana na namna ambayo aliathiriwa na mwalimu.

Mwalimu ni mtu yeyote mwenye ujuzi, ambaye anaupitisha ujuzi kwa mtu mwingine mwenye kiwango cha chini cha ujuzi. Hakika hata wewe mwanafunzi umewahi kuwa mwalimu kwa mwanafunzi hata na mwalimu wako! Fikiria mkiwa katika darasa la kwanza au la pili, namna uliyomfundisha mwanafunzi mwenzako namna ya kuchora mambo mbalimbali, kuruka kamba na hata kufunga tai. Huenda ukadhani kwamba hujawahi kumfunza mwalimu wako lolote. Hata hivyo, kumbuka kwamba wakati unapochangia lolote darasani huwa unawafunza wengine, akiwemo mwalimu, kuhusu namna ya kueleza mambo tofauti tofauti katika somo hilo kwa mtindo tofauti. Pia unaweza hata kumfunza mwalimu wako maarifa mapya. Mathalani unapopewa fursa ya kuwatumbia wenzako ngano kutoka jamii yako unapata fursa ya kumfunza mwalimu na wanafumzi wenzako kuhusu utamaduni wa jamii yako. Kupitia ngano hizi unaweza pia kumfunza namna ya utambaji.

Umuhimu wa mwalimu yeyote yule hauwezi kupuuzwa. Mwalimu humwondolea mtu ujinga kwa kumfunza maarifa mbalimbali. Wewe fikiria ulipoingia katika shule ya chekechea. Ulikuwa mgeni kabisa katika mazingira ya shule. Ulikuwa hujazoea kuishi na watu ambao si wa familia yako. Jambo la kwanza ambalo mwalimu alikufunza ni kuishi au kuwa na maarifa ya kuishi na watu wengine. Alikufunza pia namna ya kuomba msamaha unapowakosea wenzako, pamoja na kushirikana nao katika michezo mbalimbali bila kuumizana. Juu ya hayo, mwalimu alikufunza namna ya kutamka sauti ya maneno mbalimbali. Baadaye alikufunza kuzisoma sauti na maneno ya vifungu mbalimbali. Bila shaka mwalimu alikufunza kuandika na kuwasiliana kwa **mitindo anuwai.**

Licha ya kufunza masomo mbalimbali, mwalimu huelekeza kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zinaweza kuathiri masomo ya mwanafunzi. Hushauri namna ya kutafuta haki na kusuluhisha migogoro tofauti kwa amani. Mwalimu hukushauri kwamba hata mwenzako anapokukosea haifai kumtusi au kumwendea mwalimu kushtaki. Njia bora ni kumwambia kwa utulivu kuwa amekosea na kumsamehe iwapo atakuomba msamaha. Ikiwa mwenzako atashindwa kuona kuwa kosa alilokutendea, basi unaweza kumwambia mwalimu ili awaelekeze zaidi na kuwasaidia kusuluhisha tatizo lenu.

Mwalimu pia hukusaidia kutambua na kukuza vipawa vyako. Vilevile hukusaidia na kukuelekeza kutambua udaidhi wako katika masomo na hali tofauti, na kukuhimiza kutafuta mikakati ya kujiimaarisha. Mathalani, ikiwa una kipawa cha ushairi, mwalimu anaweza kukitambua kupitia nyimbo mnazoimba darasani. Kwa njia hii, anaweza kukusaidia kujiimarisha. Hakika wapo washairi stadi ambao walisaidiwa kufika kiwango hiki na mwalimu wao. Vilevile kuna wasusi ambao wameibuka kuwa hodari kwa kusaidiwa na walimu wao wa awali katika taaluma ya ususi.

Ni dhahiri kwamba binadamu hukumbana na walimu wengi maishani. Hata hivyo ni muhimu kwamba japo walimu wa kawaida huwa na nia nzuri, wakakufunza ya kufaa, kuna wengine amabao wanaweza kukufunza ya kukuhasiri. Hawa hawakufunzi kwa maneno tu, bali pia kwa vitendo. Walimu wa aina hii hukuvutia kwa vitendo vyao kwa kutumia vishawishi vingi. Polepole unajikuta umenaswa kabisa; ukawa mtumwa wao. **Si ajabu ukipata kwamba ukiandamana na marafiki ambao wameingiliana na vileo, utainukia kuwa mraibu sugu wa vileo hivi**. Hili hutokea pale ambapo, kwa kutoka kujitambulisha na marafiki zako, unawafuata namna bendera ifuatavyo upepo. Hivyo basi ni muhimu kuwa na msimamo thabiti hata tunapoingiliana na walimu wa aina mbalimbali tuchuje tunayofaa kujifunza. Yale yasiyofaa tuyaambae kama ukoma.

**31.** Chagua jibu sahihi kulingana na aya ya kwanza.
- A. Mwandishi anajua kwamba msomaji anaweza kufunza mwalimu wake
- B. Neno 'mwalimu' lina maana tofauti tofauti kulingana na wahusika
- C. Mwalimu anapofunza maarifa darasani watu wengi huyapitisha kwa wengine
- D. Akili inapojiwa na neno 'mwalimu' hurejelea maarifa

**32.** Chagua jibu lifaalo kulingana na kifungu.
- A. Watu wenye kiwango cha chini cha ujuzi hawajui maana ya maumbo
- B. Shughuli za mwanafunzi darasani ni njia ya kupitisha maarifa kwa wengine
- C. Mwanafunzi anapofungia tai darasani marafiki hujifunza kuifunga vyema
- D. Wakati watoto wanaposoma wanajua kwamba hawawezi kuwafunza wakuu wao

**33.** Kifungu kimebainisha kwamba
- A. utambaji ni njia ya kuonyesha sifa za jamii fulani
- B. wanafunzi huwa na mitindo tofauti ya kutambia familia zao
- C. mwalimu hujua utambaji anapoambiwa kuhusu ngano za wanafunzi
- D. utamaduni wa wanafunzi huimarika wanapofundishwa utambaji darasani mwao

**34.** Kulingana na aya ya tatu,
- A. maarifa anayofunzwa mwanafunzi huweza kumfanya kutompuuza mwalimu
- B. watu wakiingia shule za chekechea hawajui familia nyingine
- C. mwanafunzi anajua maana ya vifungu anapoingia shuleni
- D. mwalimu anaweza kumfanya mwanafunzi kuwa mnyenyekevu

**35.** Chagua umuhimu wa shule kulingana na aya ya tatu.
- A. Kukuza uvumilivu, kukosa makosa
- B. Kukuza utiifu, kujikinga na maumivu
- C. Kukuza mazoea ya michezoni, kuimarisha hati
- D. Kukuza utangamano, kustawisha mbinu za kujieleza

**36.** Aya ya nne imebainisha kwamba
- A. mwalimu anapotambua changamoto zinazotokana na masomo, alama za wanafunzi huimarika
- B. mwanafunzi anapoelekezwa kuhusu aina za migogoro isiyofaa huwa bora masomoni
- C. mwalimu humjengea mwanafunzi hulka ya kutafuta anacho stahili bila kuwaumiza kihisia
- D. mwanafunzi huwahimiza wenzake kujadiliana kuhusu matatizo yao kabla ya kumwarifu mwalimu

**37.** Chagua jibu sahihi kwa mujibu wa aya ya tano.
- A. Mwanafunzi anapoimba nyimbo darasani huvielewa vipawa vya wengine
- B. Mwalimu akimsaidia mwanafunzi, yeye hupata mbinu za kuimarisha vipawa
- C. Mwalimu humwelekeza mwanafunzi kujua ubora wake katika nyanja mbali mbali
- D. Mwandishi anamtegemea mwalimu wa awali kufahamu namna za wasusi shuleni

**38.** Aya ya mwisho imebainisha kwamba
- A. maarifa ayapatayo binadamu yanaweza kutokana na vielelezo anavyoona kutoka kwenya mazingira yake
- B. idadi kubwa ya walimu anapoota mtu huwa na ari ya kumsaidia ya kumwadilisha
- C. watu wengi huingia kwenye mitego ya washauri kwa kutojua athari za dawa
- D. baadhi ya wanafunzi hushirikiana na wanafunzi wanapojikuta wakiwa na ushawishi mdogo

**39.** **'Si ajabu kupata kwamba ukiandamana na marafiki ambao wameingilia matumizi mabaya ya vileo, utainukia kuwa mraibu sugu wa vileo hivi.'**
Chagua methali ambayo inajumuisha ujumbe wa kauli hii.
- A. Mshika mbili moja humponyoka
- B. Mchezea tope haliachi kumrukia
- C. Mdharau mwiba hupata tende
- D. Mpanda ovyo hula ovyo

**40.** Maana ya **'mitindo anuwai'** kulingana na kifungu ni mitindo
- A. ambayo haihusiani
- B. ya aina nyingi
- C. ya wasemaji tofauti
- D. ambayo haijapatika

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 – 50**

Okello Legea alikuwa mwanamume mwenye miraba minne, mrefu kushinda mlingoti. Yakini, **Okello angeweza kuyafikia mawingu kwa urefu wake**. Hakuwa mweusi tititi, wala wa rangi ya hudhurungi. Alipokuwa shuleni, masomo hayakumhusu ndewe wala sikio. Aliend shuleni maadamu wenzake walienda. Kazi ya kiada na ziada alizifanya tu ama kujiepushia adhabu au kuwapendeza wazazi. Alipoufanya mtihani wa darasa la nane, aliambulia alama za kufutia machozi. Licha ya hali hii kumsononoesha baba yake, alipiga moyo konde. Hakutaka kujiongeza sononeko baada ya mkewe kufumwa na mvi wa manaya.

Baba yake alizungumza na sahibu aliyemiliki shule ya upili pale kijijini. Okello akajiunga na shule ile. Baba yake **alikuwa na matumani ya tai mtini kuliokea jahazi lilokuwa likizama**. Okello Legea aliendelea kujipakatia mikono pale shuleni. Alifahamu kuwa utajiri wa baba yake ungemfaa siku za halafu. Lile ambalo hakujua ni kuwa mtegemea cha nduguye hufa maskini. **Kuufanya mtihani wa kitaifa na kutoufanya yote yalikuwa mamoja**. Baba yake alizungumza na afisa mmoja wa polisi aliyemfanyia mpango kabambe na kumsajili Okello katika kikosi cha polisi.

Katika kituo cha polisi cha Kaa Macho, Okello alitokea kuwa polisi wa kipekee. Wengi walidhani kuwa Okello aliwajali wananchi wote. Alionekana kukashifu sana wizi katika eneo hilo. Kila wakati angewaongoza maafisa wenzake kuwasaka na kuwaangamiza wezi. Wakaazi wa eneo hilo walimpenda sana. "Tungekuwa na Okello wanne hapa, uhalifu ungekuwa umemalizika." Wanaanchi wa eneo hilo walisikika wakisema.

Siku moja, usiku wa manane, palisikika kamsa kutoka kwa mzee mmoja aliyekuwa amevamiwa na wezi. Wanakijiji wenzake waliuthamini sana ujirani. Walijitia ushujaa na kwenda kumnusuru mwenzao. Waliusuka mpango mzuri na kuwanasa wezi hao ambao walikuwa wamegeuka dondandagu. Wanakijiji kadhaa walitokea nyuma ya boma. Wengine watatu nao wakaanza kupiga kelele njiani. Mwizi mmoja aliyekuwa na bunduki alianza kutembea akielekwa kule njiani. Mwizi huyo wa bunduki ndiye aliyeshikwa wa kwanza, pamoja na mwenzake wawili. Nusu ya wezi hao ndiyo iliyoshikwa.

Wezi walipomulikwa, kila mtu alipigwa na butwaa chakari. Okello alikuwa mmoja wa wezi hao walionaswa. **Kumbe uzuri wake ulikuwa tu wa mikakasi**. Alilia na kuomba msamaha ili asichomwe. Wananchi wale walitiwa upofu na hasira. Okello na wenzake walipatwa na kichapo cha mbwa. Yule wa kununua petrol alikuwa mbioni kuitafuta. Wezi sasa walikuwa wamelia hadi visima vyao vya machozi kukauka. Mara petroli ililetwa. Kama si kuwasili kwa maafisa wengine wa polisi, tungekuwa tukiongea mengine.

**41.** Mwandishi ametumia maneno, '**Okello angeweza kuyafikia mawingu kwa urefu wake.**' Ni tamathali gani ya usemi iliyotumika katika sentensi hii?
A. Kinaya B. Istiara C. Chuku D. Tashbihi

**42.** Aya ya kwanza imedhihirisha kwamba
A. Okello hakufanya kazi ya ziada na kiada
B. Okello alipenda sana shule kama wengine
C. Mama wa Okello alikuwa ameaga dunia
D. Okello alikuwa amekonda na kukondeana

**43.** Maneno '**alikuwa na matumaini ya tai mtini kuliokoa jahazi lililokuwa likizama**' ina maana kuwa
A. alikuwa amepoteza matumaini
B. maisha ya mwanawe yalikuwa yameharibika
C. baba yake alitamauka kama tai
D. maisha ya mwanawe yalikaribia kuharibika

**44.** Yaelekea kuwa wezi wote walikuwa wangapi?
A. Watatu B. Sita C. Watano D. Wanne

**45.** Kulingana na aya pili ni kweli kusema kuwa
A. Okello hakuufanya mtihani
B. baba ya Okello alimiliki shule ya upili
C. Okello alipata alama mbovu katika shule ya upili
D. Okello alitegemea cha nduguye kisha akafa maskini

**46.** Hali ya majirani kumwokoa mwenzao inadhihirisha methali gani?
A. Siku za mwizi ni arubaini
B. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
C. Jambo usilolijua ni kama usiku wa giza
D. Ujanja wa nyani huishia jangwani

**47.** Siku za halafu ni siku gani kulingana na kifungu?
A. Siku za kisogoni C. Siku za baadaye
B. Siku za starehe D. Siku zilizopita

**48.** '**Kumbe uzuri wake ulikuwa wa mkakasi**' ndiko kusema;
A. Alionekana mzuri nje kumbe ndani alikuwa mbaya
B. Uzuri wake ulikuwa wa kumwezesha aibe
C. Alikuwa mzuri kama mkakari
D. Alikuwa polisi aliyeiba usiku

**49.** Kulingani na aya ya tatu ni kweli kusema kuwa
A. Okello alikuwa pekee yake katika kituo cha polisi
B. Okello alikuwa tofauti na wenzake katika kituo cha polisi
C. Okello alikashifiwa na wezi katika kituo cha polisi
D. Okello walikuwa wanne katika kituo cha polisi

**50.** Mwishoni wa kisa hiki
A. Okello na wenzake walichomwa
B. Okello na wenzake walitoroka
C. Okello na wenzake waliokolewa na polisi
D. Okello na wenzake waliuawa.